# JARIBIO LA MTIHANI WA LUBINU /LUSHEYA

## DARASA LA NANE MUHULA WA KWANZA – 2020

**KISWAHILI**

**Muda: Saa 1Dakika 40**

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

1. Tumia penseli ya kawaida.
2. Hakikisha umeandika kwenye karatasi ya majibu:-
   **(i) JINA LAKO** **(ii) JINA LA SHULE YAKO**
3. Kwa kila swali, onyesha jibu sahihi kwa kuchora kijistari kwenye mabano ya alama ambayo umeichagua kuwa ndilo jibu sahihi.

***Soma vifungu vifuatavyo vina nafasi 1-15. Umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

Je – 1 – wajua ni haki ya kila mtoto kupata elimu? Ni kwa kutambua jambo hili – 2 – serikali ya Kenya ilitangaza kuwa itatoa elimu ya – 3 – kwa watoto wote, ili kila – 4 – apate nafasi ya kujipatia elimu ya msingi. Hali kadhalika, watoto wa – 5 – wa kuenda shuleni hawapaswi kuajiriwa mahali – 6 – pale. Yafaa watunzwe vyema ili – 7 -, waelimike na wawe viongozi bora wa siku za – 8 -.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. , | B. ? | C. ! | D. . |
| 2. | A. ambako | B. ambao | C. ambaye | D. ambapo |
| 3. | A. lazima | B. dezo | C. kawaida | D. hiari |
| 4. | A. moja | B. mmoja | C. mumoja | D. mojawapo |
| 5. | A. rika | B. kimo | C. kiwango | D. umri |
| 6. | A. pote | B. kokote | C. popote | D. kote |
| 7. | A. wawe | B. wakue | C. wasiwe | D. wale |
| 8. | A. kiyama | B. kisogoni | C. zama | D. usoni |

Tofauti za kisiasa na kikabila – 9 – kuliangamiza taifa letu. Waja wamejawa na chuki – 10 – wenzao. – 11 – kila mmoja anaona kwamba mtu wa kabila – 12 – ni adui yake. – 13 – na hali hii huenda uchumi wetu – 14 – kabisa. Vijana – 15 – tegemeo la kulikomboa taifa hili.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 9. | A. linatishia | B. zinatishia | C. inatishia | D. zinatisha |
| 10. | A. kati ya | B. miongoni mwa | C. mithili ya | D. dhidi ya |
| 11. | A. ambayo | B. ambapo | C. ambao | D. ambavyo |
| 12. | A. ingine | B. nyingine | C. jingine | D. kingine |
| 13. | A. Tulienda | B. Tukienda | C. Tukiendeleza | D. Tukiendelea |
| 14. | A. ukasambaratika | B. likasambaratika | C. ikasambaratika | D. tukasambaratika |
| 15. | A. ndilo | B. ndio | C. ndiyo | D. ndiye |

***Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu sahihi kulingana na maagizo uliyopewa.***

16. Andika wingi wa udogo wa sentensi hii:
    Mbwa wamepatikana ndani ya nyumba
    A. Vijibwa wamepatikana ndani ya vijumba
    B. Vijibwa vimepatikana ndani ya vijumba
    C. Mbwa wamepatikana ndani ya nyumba
    D. Vijibwa vinapatikana ndani ya nyumba
17. Sentensi ipi yenye kiambishi 'ki' cha masharti
    A. Huko hakukaliki
    B. Tulikuwa tukisoma
    C. Wakifika watanipata
    D. Nimekiona kitabu chenyewe
18. $^6/_9$ kwa maneno ni___
    A. Sudusi sita B. Tusui tisa
    C. Sudusi tisa D. Tusui sita
19. Asiyesikia la mkuu huvunjika guu. Kiwakilishi ni kipi katika sentensi hii?
    A. la B. asiyesikia
    C. huvunjika D. guu

20. Kanusha: Ningekuwa hapo angekubali kwenda.
  A. Ningekuwa hapo hangekubali kwenda
  B. Ningekuwa hapo asingekubali kuenda
  C. Nisingalikuwa hapo asingekubali kuenda
  D. Nisingekuwa hapo asingekubali kuenda

21. Mkono wazi ni kwa ukarimu ilhali _____ ni kwa inda.
  A. joka la mdimu
  B. kiunga ungo
  C. jicho la nje
  D. kisebusebu

22. Jina wanaloitana ndugu wa kike na wa kiume ni:
  A. umbu
  B. somo
  C. mnuna
  D. kaka

23. "Unamtafuta mwalimu _____ shuleni?" Mzazi aliulizwa.
  A. wapi
  B. mpi
  C. gani
  D. mgani

24. Andika sentensi hii katika usemi wa taarifa.
"Siondoki hapa mpaka nimwone mtoto wangu," mama alisema.
  A. Mama alisema kuwa asingeondoka hapo mpaka amwone mtoto wake
  B. Mama alisema hataondoka pale mpaka atakapomwona mwanawe
  C. Mama alisema asingeondoka hapa mpaka amwone mtoto wangu
  D. Mama alisema mpaka nimwone mwana wangu siondoki hapa.

25. Nomino 'shida' hupatikana katika ngeli gani?
  A. LI – YA
  B. U – ZI
  C. I – I
  D. I – ZI

26. Nyumbani ambapo anakaa _____ nakarabatiwa
  A. ku
  B. m
  C. pa
  D. I

27. Neno darasa lina silabi ngapi?
  A. Tatu
  B. Sita
  C. Mbili
  D. Moja

28. Chagua wingi wa sentensi ifuatayo.
Mchungaji alinitunzia mbuzi huyu wangu huko kwake.
  A. Wachungaji walinitunzia mbuzi hawa wangu huko kwao.
  B. Wachungaji walinitunzia mbuzi hawa wangu huko kwake
  C. Wachungaji walitutunzia mbuzi hawa wetu huko kwao.
  D. Mchungaji alinitunzia mbuzi hawa wetu huko kwao

29. Chagua sentensi iliyo katika hali timilifu
  A. Ninakula chakula hiki
  B. Vyote havipendezi
  C. Tulichelewa kufika
  D. Tumefika shuleni mapema

30. Sifa kutokana na kitenzi cheka ni _____
  A. cheshi
  B. kicheko
  C. chekesha
  D. ucheshi

***<u>Soma ufahamu ufuatao kisha ujibu maswali 31 – 40.</u>***

Baada ya kumaliza darasa la nane Ndawaki aliamua kuanza kiwanda kidogo cha useremala. Ingawa wazazi wake hawakuweza kumlipia karo ya shule ya upili walijitahidi kumtafutia mtaji wa kufungua kazi aliyotaka.

Alipopata mtaji, Ndawaki alikarabati duka moja pale pao kijijini na kununua zana za useremala. Alinunua vifaa kama vile msumeno, nyundo, spana, bisibisi, kekee, utepe, randa na patasi. Alijipatia malighafi kama bao. Hamu yake kubwa ilikuwa kutengeneza samani kama vile makochi, viti, vitanda na kabati. Alitaka kuvisanii kwa njia ambayo ingemfurahisha mtumiaji daima dawama.

Hamu yake ya kutengeneza bidhaa hizi ilididimia alipopewa kazi na mteja wake wa kwanza. Mteja huyu alitaka atengenezewe jeneza! Kwa kweli utengenezaji wa jeneza ni jambo ambalo Ndawaki hakuwa amefikiria. Hakuwa na hamu ya kuunda kitu ambacho mtumiaji hangekiona wala kufurahia.

Kwa vile ilikuwa mara yake ya kwanza kuunda jeneza, fikra za kifo zilimjia mara kwa mara alipofanya kazi ile. Alitengeneza kwa huzuni mwingi.

Siku ya pili alitembelea kibanda cha jirani yake aliyejishughulisha na uuzaji wa vipuri pamoja na ukarabati wa magari. Jirani huyu alikuwa na tajiriba ya siku nyingi na alikuwa

amejiimarisha kwa kununua vifaa vya kisasa kama vile tarakilishi ya kuhifadhia rekodi zake, rununu ya kuwasiliana na jenereta ya kutumia nguvu za umeme zilipokosekana.

Ndawaki alishtuka sana jirani yake alipomwelezea kuwa gari alilokuwa anatengeneza ndilo lililohusika katika ajali iliyosababisha kifo cha aliyekuwa anayetengenezewa jeneza. Sadfa gani hii? Ndawaki alishangaa.

Jirani yake aliendelea kumweleza kuwa mambo kama yale yalileta nafuu kwa wenye viwanda kwa vile yaliwapa kazi, kweli vita vya panzi furaha ya kunguru.

Ilikuwa vigumu kuamini maneno ya jirani yake. Siku za mwanzo lakini baadaye Ndawaki alizoea kazi viwandani.

31. Chagua jibu ambalo si sahihi.
Ndawaki alianza useremala ___
   A. wazazi wake walipompa mtaji
   B. alipomaliza darasa la nane
   C. alipomtembelea jirani
   D. alipokosa kwenda shule ya upili
32. Ni gani ambayo ni tofauti kikazi?
   A. Kikaango B. Spana
   C. Nyundo D. Msumeno
33. Mahali panapotengenezwa bidhaa huitwa___
   A. kipuri B. kipanda
   C. kiwanya D. kiwanda
34. Tarakilishi haitumiwi ___
   A. kuweka rekodi B. kupiga randa
   C. kufanyia hesabu D. kupigia chapa
35. Neno lingine lenye maana sawa na samani ni _
   A. zamani B. kale
   C. makochi D. fanicha
36. Kwa nini Ndawaki hakupenda kutengeneza jeneza?
   A. Ilikuwa kazi ngumu kutengeneza jeneza
   B. Mtumiaji hangeweza kuliona wala kulifurahia
   C. Aliona kama kifo kingemjia
   D. Ilikuwa si mara yake ya kwanza kulitengeneza
37. Jirani ya Ndawaki alikuwa na vifaa kama vile___
   A. Vipuri, tarakilishi na tajiriba
   B. Tajiriba, vipuri na jenereta
   C. Jenereta, tarakilishi na vipuli
   D. Ukarabati, magari na vipuri
38. Mali aliyohitaji ili kuanzisha kazi ni:
   A. mtaji B. mteja
   C. malighafi D. fedha
39. Kazi ya viwandani yaelekea ___
   A. hukidhi mahitaji ya fundi pekee
   B. haihitaji nguvu nyingi
   C. hukidhi mahitaji ya jamii
   D. ni ya kushangaza sana
40. Methali "vita vya panzi furaha ya kunguru" imetumika hapa kumaanisha ___
   A. Hasara ya wengine inaweza kuwa faida ya wengine
   B. Faida ya wengine inaweza kuwa hasara ya wengine
   C. Kazi ya viwandani inahitaji uvumilivu
   D. Kazi ya viwandani huleta nafuu

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41-50.**

Katika pilikapilika za maisha, wanadamu hujipata katika hatari mbalimbali.

Ajali za ghafla huweza kutokea au hata maradhi yasiyotarajiwa. Hali kama hii huhitaji huduma ya dharura ili kuzuia upotezaji wa maisha. Huduma ya kwanza ni mojawapo ya usaidizi wa kwanza anaopewa mtu ambaye amepatwa na ugonjwa au ajali ya ghafla.

Huduma ya kwanza inajihusisha na kutunza maisha na kuzuia hali kuwa mbaya zaidi kabla ya majeruhi au mkongo kupata usaidizi wa tabibu. Wanaotekeleza huduma ya kwanza hupata mafunzo kuhusu matibabu ya kimsingi yanayohitajika kwa wingi. Si madaktari hasa ingawa wanaweza kufunga mahali ambapo pamekatwa, kupulizia magonjwa hewa aliye na tatizo la kupumua, kuondoa walio hatarini kuumizwa na kukimbiza hospitalini walioumia zaidi.

Haya tu ni baadhi ya yale yanayofanywa na wale wanaotoa huduma ya kwanza.

Nchini Kenya, kuna mashirika yanayojihusha na utoaji wa huduma ya kwanza kama vile shirika la msalaba mwekundu, St. John Ambulance na huduma ya kwanza ya St. Andrew. Baadhi ya mashirika haya huwapa mafunzo watu waliojitolea kuwa wahudumu wa huduma ya kwanza. Wapo wanafunzi pamoja na walimu waliojitolea kuwahudumia wenzao walioumia au kupatwa na ugonjwa wa ghafla baada ya kupata mafunzo ya kimsingi.

Katika mazingira ya shule, hatari zinazoweza kuhitaji huduma ya kwanza ni pamoja na moto wa ghafla au uvamizi wa magaidi. Kwa kuwa huduma ya kwanza inahusu utabibu wa kimsingi, ni muhimu kuwepo na vifaa vinavyohitajika katika shughuli hii. Mwalimu anayeongoza utoaji wa huduma ya kwanza anafaa kumwelekeza mwalimu mkuu kununua vifaa vinavyohitajika. Ikiwezekana, kila mwanafunzi apate mafunzo ya kimsingi kuhusu vile anavyoweza kujisaidia akiwa hatarini au hata kumsaidia mwenzake. Wote wakiwa na ufahamu wa huduma ya kwanza, shule zitaepukana na hatari zinazotokea kila mara na kusababisha maafa.

Kwa hakika, huduma ya kwanza ni muhimu katika maisha ya binadamu. Nyumbani, mahali pa kazi, barabarani, kwenye burudani na kokote kule kuliko na uwezekano wa hatari kutokea. Ikiwezekana, somo la huduma ya kwanza lafaa kuanzishwa shuleni na kuambatanishwa na lile la elimu ya maisha.

41. Kulingana na aya ya kwanza___
   A. pilikapilika za mwanadamu kila siku ni hatari
   B. binadamu hupata ajali kila siku
   C. mwanadamu hukabiliwa na hatari nyingi maishani
   D. shughuli zote za binadamu huwa hatari

42. Huduma ya kwanza ni___
   A. msaada unaotolewa mwanzoni ili kuzuia majeraha
   B. matibabu yanayotolewa mwanzoni ili kupunguza ajali
   C. msaada anaopewa majeruhi kwanza na daktari
   D. msaada unaotolewa mwanzoni ili kuokoa maisha

43. Yeyote aliyejeruhiwa anajulikana kama ___
   A. majeruhi B. mgonjwa
   C. jeraha D. mjeruhi

44. Wote wanaohusika katika utoaji wa huduma ya kwanza___
   A. sharti wapitie mafunzo ya udaktari
   B. huhitaji kupata mafunzo ya kimsingi katika uokoaji
   C. wote hufanya hivi kwa ada fulani
   D. ni madaktari ingawa hawana ujuzi wa kutosha

45. Yupi asiyehitaji kupewa huduma ya kwanza?
   A. Mja aliyezirai
   B. Aliyetangulia mbele ya haki
   C. Aliyekatwa jeraha kubwa
   D. Aliyechomeka na moto

46. Mashirika yanayotoa huduma ya kwanza nchini Kenya si pamoja na___
   A. St. John Ambulance
   B. Shirika la msalaba mwekundu
   C. Wananchi wa kujitolea
   D. St. Andrew

47. Kulingana na aya ya nne___
   A. ni kawaida ya wanafunzi kupigana na kuumizana
   B. shule nyingi zimewahi kushambuliwa na magaidi
   C. baadhi ya michezo husababisha majeraha
   D. huduma ya kwanza huhitajika na walio motoni

48. Ni vyema kwa kila mwanafunzi kupata mafunzo ya kimsingi ya huduma ya kwanza ili ___
   A. aweze kuwafaa wenzake nyumbani
   B. ajifae yeye na wenzake popote
   C. awe na msingi wa kusomea udaktari
   D. kuzuia uwezakano wa kutokea ajali shuleni

49. Ajali kwa kawaida huleta ___
   A. maafa B. hasara
   C. upweke D. wasiwasi

50. Maoni ya mwandishi katika aya ya mwisho ni kuwa ___
   A. ajali inaweza kutokea mahali popote
   B. ajali hutokea nyumbani, kazini na barabarani
   C. somo la huduma ya kwanza ni lazima shuleni
   D. elimu ya huduma ya kwanza si muhimu kama mengine